



OFISI YA RAIS,
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA MKURANGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MDC/T.10/11/113

18 Februari, 2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA ANWANI YA
MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga anapenda kuwatangazia nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la Anwani za Makazi katika Kata na Vijiji vya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- (i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 – 35
- (ii) Awe na elimu kuanzia kidato cha Nne na kuendelea
- (iii) Awe anamiliki simu janja, Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- (iv) Awe na barua pepe (email) na nywila (password) inayofanya kazi.
- (v) Awe na uwezo wa kusoma ramani za Vijiji.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- (ii) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma
- (iii) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia Mfumo wa Anwani za Makazi.
- (iv) Kutuma data kwenye Mfumo wa Anwani za Makazi.

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;

- (i) Nakala ya cheti cha kidato cha Nne na kuendelea
- (ii) Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- (iii) Picha (Passport size 2)
- (iv) Barua ya maombi ipitie kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji alichopo muombaji.
- (v) Hakikisha unataja namba zako za simu ya mkononi.

D. MALIPO

Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku.

E. JINSI YA KUTUMA MAOMBI


Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba za simu, barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Afisa Mtendaji wa Kata kwa anwani ifuatayo:

Afisa Mtendaji wa Kata,
Kata (taja Kata uliopo),
S.L.P 10,
MKURANGA.

F. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 25/02/2022 saa 9:30 Alasiri.

Limetolewa na;


Mwantum H. Mgonja
Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya
MKURANGA

